

HABARI KASKAZINI

UWEKEZAJI

TASAF yaombwa kuongeza uwekezaji

Na Renatha Msungu, DODOMA

MLENGWA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), Pili Selemani ameiomba serikali kuongeza uwekezaji kwenye mfuko huo ili kuendelea kuwaondoa wananchi kwenye umaskini kwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali.

Pili alitoa ombi hilo jana jijini hapa katika Maonesho ya Kilimo kitaifa kwa mwaka huu yanayoendelea katika Viwanja vya Nzuguni mkoani Dodoma.

Alisema mfuko huo ni msaada mkubwa kwa jamii kwa kuwatoa baadhi ya wananchi kwenye umaskini na kufikia hatua ya kula milo mitatu.

Akisimulia TASAF ilivyomwinua kimaisha kupitia fedha anazopewa na mfuko huo, ameondokana na ufukara baada ya kuanzisha mradi wa ujasiriamali na kupata fedha za kumunua chakula na kusomesha watoto.

Mfuko huo ni msaada mkubwa kwa jamii kwa kuwatoa baadhi ya wananchi kwenye umaskini na kufikia hatua ya kula milo mitatu.

Marium Kassim, alisema mfuko huo umemtoa katika umaskini na kuwa mjasiriamali wa bidhaa mbalimbali na kupata kipato cha uhakika kuendesha maisha yake.

Mariamu aliwataka wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi katika maonesho hayo kujifunza namna ya kutengeneza bidhaa na kuinuka kiuchumi.

Aliiomba Serikali kuwapatia vitendea kazi kwa ajili ya miradi waliyoanzisha ya ujasiriamali na kukuza biashara zao.

Mwakilishi wa TASAF, Melkizedek Nduye, aliwataka wadau kujitokeza kwa wingi katika banda la mfuko huo kujifunza mambo mbalimbali, ikiwemo kuondokana na umaskini.

Nduye, alisema TASAF pamoja na kutoa fedha kwa walengwa, imekuwa ikitoa elimu kwa walengwa wa mpango huo namna ya kutumia na kujitegemea kupitia ujasiriamali.

MAPATO

TANAPA yajivunia kukusanya 500b/-

Na Godfrey Mushi, BABATI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limepata mafanikio makubwa baada ya kuvuka lengo kwa kukusanya Shilingi bilioni 500

